



Wamepata ushindi wenyewe kujitenga

Kutoka kwa Abuu Huraira -Radhi za Mwenyezi Mungu ziwe juu yake- amesema: Alikuwa Mtume wa Mwenyezi Mungu rehema na amani ziwe juu yake akitembea katika njia ya kuelekea Makka, akapita karibu na mlima Jumdan, akasema: "Tembeeni huu ni mlima Jumdan, Wamepata ushindi wenyewe kujitenga" Wakasema: Ni akina nani hao wenyewe kujitenga ewe Mtume wa Mwenyezi Mungu? Akasema: "Ni wenyewe kumtaja Mwenyezi Mungu kwa wingi katika Wanaume, na wenyewe kumtaja Mwenyezi Mungu kwa wingi katika wanawake."

[Sahihi] [Imepokelewa na Imam Muslim]

Mtume rehema na amani ziwe juu yake ameeleza nafasi ya wale wanaomkumbuka Mwenyezi Mungu kwa wingi, na kwamba wao ni wa kipekee na wametangulia wengine katika kufikia daraja za juu katika Bustani za neema, na akawafananisha na mlima Jumdan ambao ni wa kipekee ukilinganisha na milima mingine.

<https://sunnah.global/hadeeth/sw/show/3719>

